**JAMHURIYAMUUNGANOWATANZANIA**
**OFISIYARAISI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILA YA BUTIAMA**
**SHULE YA SEKONDARI YA BUTUGURI,**


NAMBA ZA SIMU: 0757079196
MKUU WA SHULE: 0685079195
MAKAMU MKUU WA SHULE: 07555196106
S.L.P.1085, BUTIAMA-MARA.


KUMB: BSS/S.2320/2026/VOLIV/20 ……/…../……..

Ndugu; MZAZI/MLEZI WA……………………………………………………………..
S.L.P.-……………………………

YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI BUTUGURI</u> ILIYOPO HALMASHAURI YA WILAYA BUTIAMA MKOANI MARA MWAKA ………………………

**Mzazi/ Mlezi wa mwanafunzi …………………………………….**
**S.L.P ………………………..**
**……………………………….**

Ninayo furaha kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa Kujiunga na kidato cha tano katika shule ya sekondari hii na atasoma mchepuo wa HKL/ HGK/HE/HGL.

Shule ya Sekondari Butuguri ipo wilayani Butiama mkoani Mara Katika kijiji cha KISAMWENE karibu na mji wa Butiama. Endapo utatumia barabara itokayo Mwanza Au Tarime utateremkia kituo kikuu cha mabasi cha Bweri Musoma, hapo utapata magari madogo aina ya hiace yaendayo Nyamswa, kupitia KISAMWENE na yatakushusha BUTUGURI CENTRE-KISAMWENE. Wale wanaotokea **DAR ES SALAAM** wapande mabasi ya **HAPPY NATION, KAPRIKON, ALLY'S STAR** na **JOHANVIA** na Wale wanaotoka Tanga, Manyara, Kilimanjaro na Arusha kwa kupitia barabara ya Serengeti wapande mabasi ya COASTLINE, KIMOTCO, LOLIONDO au SERENGETI, watatelemkia mji wa Butiama na watachukua bajaji au pikipiki hadi shuleni. Hata hivyo baadhi ya mabasi yanapita karibu na shuleni yakielekea Musoma mjini.

Muhula wa masomo kwa wanafunzi wa kidato cha tano utaanza tarehe …………... Hivyo wanafunzi wote waliopangwa kujiunga na kidato cha tano kwa mwaka ………….. wanapaswa kuanza kuripoti shuleni kuanzia tarehe ………………. Tafadhali jitahidi kufika shuleni tarehe iliyopangwa

**4. KAULI MBIU**
Kauli mbiu ya Shule yetu ni **EDUCATION FOR TECHNOLOGY.** Hii ina maana kuwa Elimu ndiyo msingi wa maendeleo Kiteknolojia, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Daima usiridhike na kiwango cha elimu ulichonacho, jaribu tabia ya kutamani kujifunza ili kuwa na maendeleo ya juu zaidi yatokanayo na juhudi, juhudi Katika masomo maarifa na nidhamu ili kuleta ufanisi na uwezo mkubwa wa kupambana na mazingira unayoishi.
Ili kufanikisha kauli mbiu hii kila mwanafunzi atatakiwa kujiheshimu, kuwaheshimu walezi/walimu na wanafunzi wenzake, kufanya kazi kwa bidi ndani na nje ya darasa, kujirekebisha Katika mwenendo, tabia na nidhamu.

Kwa heshima uliyopewa ya kuchaguliwa kujiunga na shule hii, unategemewa sana na shule, wenzako na jamii nzima ya hapa kuwa kielelezo kizuri cha shule yetu na Taifa kwa ujumla. Kanuni na sharia za shule zilizo ambatanishwa hapa zitakusaidia kufikia malengo yako. Kauli mbiu ya shule na madhumuni yako ya kuja hapa ni mwanga sahihi wa maisha yako ya baadaye. **ZISOME KWA MAKINI SANA** na ufahamu kuwa kusoma ni kujifunza na kujifunza ni kufahamu, kufahamu ni kujituma na kujituma ni kazi na kazi ni uhai wako kwa jamii na Taifa.

**B. MAHITAJI YA SHULE**

**I. MAHITAJI YA KUJA NAYO MWANAFUNZI**

1. Godoro 1 la ft 3 unene wa nchi nne linalo faa kwenye kitanda cha chuma.
2. Shuka 3, mbili za pink zisizo na maua au mapambo na moja ya blue
3. Foronya 2. Moja ya pink na moja ya blue
4. Blanketi 1 kwa ajili ya baridi
5. Mwanafunzi aje na track suit rangi ya kijivu
6. Ndoo 2 moja ya lita10 na yapili lita 20 na dishi moja kwa matumizi yako binafsi.
7. Vyombo vya chakula; sahani (isiyoyabati), bakuli, kikombe, kijiko, kidumu cha lita tano kwa ajili ya maji ya kunywa.
8. Mwanafunzi aje na vifaa kwa ajili ya usafi wa ndani na nje, vifaa hivyo ni:-
   Hard bloom na mfagio kwa HGK, Squezer na mfagio kwa HKL, Mopper na mfagio kwa HGL.
9. Aje na madaftari ya kutosha masomo yote na begi la mgongoni la kubebea madaftari. Pia yanapatikana katika duka la shule
10. Ream paper 2 za (A4 ) aina ya Double A
11. Jalada tupu 2 (file) moja liwe box file na lingine liwe spring file kwa ajili ya kuhifadhi nyaraka zake na kumbukumbu za mitihani.
12. Kanga/kitenge jozi mbili kwa ajili ya matumizi binafsi.
13. mwanafunzi aje na dawa ya chooni lita 5
14. Taa ndogo ya solar kwa matumizi binafsi, itamsaidia pindi umeme utakapo katika. Hii ni lazima
15. Aje na sanduku la bati/mbao na sio mabegi na masanduku makubwa ya thamani kubwa.
16. Mwanafunzi mwenye bima ya afya aje nayo
17. Mwanafunzi aje na vitabu vya masomo atakayo soma kwa matumizi binafsi.

**II. MICHANGO**

| | |
|---|---|
| 1.Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000= |
| 2.Tahadhari | 5,000/= |
| 3. Fedha ya kitambulisho na picha | 5,000/= |
| 4. Fedha kwa ajili ya nembo ya shule | 5,000/= |
| JUMLA KUU | 80,000/= |

NB: Fedha zote ziwekwe kwenye akaunti ya shule NO.30301200335 **NMB *BUTUGURI SECONDARY***. Mwanafunzi anatakiwa aje na Bank Paying Slips.

**III. SAREYASHULE.**

1. Mashati 2 ya tetron meupe yenye mikono mirefu. Mashati yanayo bana hayaruhusiwi.
2. Aje na sketi 2 rangi ya **DAMU YA MZEE** (kitambaa kizito) iliyo kolea yenye malinda 6, mbele linda kubwa na nyuma linda kubwa pembeni madogo na zipu upande wa kulia. Sketi hizo ziwe ndefu mpaka chini kwenye kifundo cha mguu. Sketi hizo mbili (2) ni kwa ajili ya masomo darasani. Rejea picha

no_01 kwa wanafunzi wa kiislam waje na juba la rangi **NYEUPE** kwa darasani na **NYEUSI** kwa ajili ya kushindia hiyo lisiwe na maua ya aina yoyote au urembo. Juba lifike kwenye kiwiko cha mkono.

3. Tisheti, tai na sweta lenye nembo ya shule
4. Raba nyeupe na t-shirt ya blue kwa ajili ya michezo.
5. Anatakiwa kushona sketi **2 dark blue** kitambaa kizito kwa ajili ya kuvaa baada ya masomo. Sketi hizo ziwe zenye malinda ya kati au wastani na zipu pembeni pia ziwe ndefu mpaka chini kwenye kifundo cha mguu.
6. Aje na chandarua cheupe au blue.
7. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi. Rejea picha no_02
8. Nguo za nyumbani **HAZIRUHUSIWI** na wakati wa kuripoti aje akiwa amevaa sare ya shule. Tarakibu

(Sample)



Picha no_01



Picha no_02

## C. MAELEZO KUHUSU SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE

**1.RUHUSA** (i) **Kwenda nje ya shule;**

Mwanafunzi haruhusiwi kwenda nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa shule/Makamu mkuu wa shule. Kuna form maalum kwa ajili ya ruhusa za wanafunzi kwa ajili ya kwenda nje ya shule kwani shule yetu ni ya bweni. Endapo mwanafunzi ataruhusiwa kwenda nje ya shule atatakiwa kuvaa sare za shule.

(ii)**Ndani ya shule;**

Ni marufuku mwanafunzi kutembelea nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu. Mwanafunzi ataruhusiwa kwenda kwenye nyumba ya mtumishi kwa ruhusa itakayotolewa na Matron baada ya kuridhika na sababu inayompeleka mwanafunzi huyo kwa mtumishi. Mwanafunzi atakaye kiuka utaratibu wa ruhusa uliowekwa adhabu yake ni pamoja na kurudishwa nyumbani na hata kufukuzwa shule.

**2.UTARATIBU WA CHAKULA**

Huduma ya Chakula hutolewa Katika bwalo la shule, mwanafunzi anatakiwa kufuata utaratibu uliowekwa kama ifuatavyo;

i. Anatakiwa kuwahi mara asikiapo kengele ya chakula.
ii. Hatakiwi kuvaa kanda mbili, nguo za michezo, kofia, na kufunga kanga ama kitenge.
iii. Shule haina utaratibu wa utoaji wa chakula maalumu (special Diet), shule inajitahidi kutoa chakula kizuri na chakuridhisha kwa wanafunzi wote kulingana na uwezo wa kifedha.

**3. NGUO ZA NYUMBANI HAZIRUHUSIWI**
Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani. Mwanafunzi atatakiwa kushindia nguo za kazi (shamba dress) hivyo anapaswa kuja na sanduku dogo tu la bati/mbao kwani hakuna sehemu ya kutunzia masanduku makubwa.

**4. AFYA**

i. Kila mwanafunzi anatakiwa kupimwa afya yake Katika hospitali ya serikali amba podaktari atatakiwa kujaza fomu iliyoambatanishwa na barua hii.

ii. Huduma za matibabu: Kila mwanafunzi atagharamia matibabu yake mwenyewe hivyo mzazi anapaswa kutoa hela ya matibabu, kwa mwanafunzi ambayo ataitunza yeye mwenyewe (mwanafunzi)

iii. Mwanafunzi atakapo ugua atapelekwa hospitalini hivyo gharama zote za matibabu zitalipwa na mzazi mwenyewe. Ili kurahisisha huduma ya matibabu, mwanafunzi aje na kadi ya bima ya afya.

**MUHIMU*** ***BIMA YA AFYA NI LAZIMA KWA KILA MWANAFUNZI***

**5. MAWASILIANO**
Mawasiliano yoyote kati ya mwanafunzi na mzazi ni lazima yapitie kwenye ofisi ya Mkuu wa Shule kwa simu namba

- **0629896267** (MKUU WA SHULE)
- **0755196106(**MAKAMU) • • **0620 564 514** (MATRON) • **0768447680 (**MATRON)

**6. LIKIZO**
Kila mwanafunzi anatakiwa arudi nyumbani kwa wazazi/walezimara tu shule inapofungwa kwa utaratibu utakao andaliwa na shule, hivyo ni vyema mwanafunzi akalipa nauli mapema ili atunziwe na shule kuepuka usumbufu wa kukosa nauli mara shule inapofungwa. Likizo inapoisha mwanafunzi anatakiwa aripoti shuleni tarehe ya kufungua shule bila kukosa.

**7. MASOMO**
(i)Madarasa na maktaba ndizo sehemu sahihi za wanafunzi kujisomea, ni marufuku kwa mwanafunzi kupiga kelele Katika maeneo hayo pindi masomo yanapoendelea. Masomo yote huendeshwa kwa lugha ya kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili. Hivyo lugha ya kuiingereza ndiyo lugha ya mazingira ya shule (lugha ya mawasiliano).

(ii**) RATIBA**
Ratiba ya shule kila siku huanza saa11:00 alfajiri ambapo kila mwanafunzi huamka ili aweze kuamka kwenda darasani. Na jioni ratiba huishia saa nne (4:00) usiku, wanafunzi wanaporudi kulala.

**8. MALEZI**
Shule ina utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba vijana wanalelewa Katika mwenendo na tabia nzuri kwahiyo tunataka mzazi uelewe kuwa wakati binti yako yuko hapa shuleni ataangaliwa kwa ukaribu sana kuhakikisha kuwa afya, tabia, mwenendo na nidhamu yake inakuwa nzuri. Hivyo shule imeandaa utaratibu ufuatao: -

***(i)Vitu vya gharama;*** Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kuja na vitu vya gharama kama vile: simu za mkononi, redio, tv, pasi ya umeme na heater. Ni marufuku kuonekana na vitu kama hivi shuleni. Endapo atakamatwa na vitu kama hivi vitaharibiwa mbele ya wanafunzi, na mwanafunzi kurudishwa nyumbani au hata kufukuzwa shule.

(ii) ***Imani***

Madhehebu ambayo hayakurasimishwa na serikali hayata tambuliwa shuleni isipokuwa kwa kibali maalumu cha serikali. Pamoja na hilo kila mwanafunzi anatakiwa aje na barua ya utambulisho kutoka kwa kiongozi wa dhehebu lake mfano, Padre, Mchungaji, Sheikh n.k.

Kila mwanafunzi ataruhusiwa kusali kwenye dhehebu lake hapa hapa shuleni kwa utaratibu wa dhehebu lake kwa kuzingatia sharia za shule.

**9. NYIMBO**

Kila mwanafunzi anatakiwa afahamu nyimbo zifuatazo na kuziimba kila anapohitajika kufanya hivyo

(i)Wimbo wa Taifa

(ii)Tanzania nakupenda kwa moyo wote

(iii)Tazama ramani

(iv)Wimbo wa shule

(v)Wimbo wa Afrika mashariki.

**10. MAVAZI**

Mwanafunzi atavaa nguo rasmi muda wote ndani na nje ya shule, akiwa amevaa sare za shule Mwanafunzi haruhusiwi kujiremba kama vile:- kuvaa hereni, bangili, mikufu, kupaka kucha rangi, kusuka, au kupaka wanja.

**11.USAFI**

(i). Kila mwanafunzi atatakiwa kuwa msafi yeye binafsi na kutunza mazingira ya shule na mahali pake anapoishi.

(ii) wanafunzi hawaruhusiwi kusuka.

(iii).Kila mwanafunzi atakabidhiwa miti ya kutunza hadi atakapomaliza shule, hii itakwenda sambamba na eneo lake la usafi.

**12. SHERIA**

Makosa yafuatayo yanaweza kumfukuzisha mwanafunzi shule hivyo ni vyema mwanafunzi akasoma na kuelewa:-

i. Kupiga/ kupigana/ kupiganisha

ii. Kumtukana mwalimu, mfanyakazi, au kiranja

iii. Wizi wa binafsi au mali ya umma/shule.

iv. Kutoroka shuleni

v. Kuvuta bangi, sigara au madawa yakulevya. vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma. vii. Kuchezea, kudharau, kuharibu fedha, bendera ya taifa au picha za viongozi. viii. Kukataa adhabu uliyopewa na kiranja, mwalimu au mkuu wa shule ix. Uasherati na usagaji x. Ubakaji xi. Kutoa mimba xii. Makosa ya jinai xiii. Kuchochea/kuongoza mgomo au kuvuruga Amani na usalama wa jamii xiv. Makosa yote yaliyothibitishwa na mahakama xv. Ni marufuku mwanafunzi kushiriki kuuza kitu chochote ambacho ni mali yake au ya shule akiwa shuleni.

- ***Kufukuzwa shule kwa mwanafunzi ni uamuzi wa kamati ya nidhamu uliothibitishwa na bodi ya ushauri ya shule.***

13**. KUWASILI SHULENI**
i. Ingia ofisi ya makamu mkuu wa shule kwa usajili ii. Ingiaofisiyamhasibukufanyamalipokamailivyoelekezwakwenyebarua iii. Ripoti kwa mwalimu wa taaluma kwa ajili ya kupewa meza na kiti.

Njoo na vitu vifuatavyo:-

a. Joining instructions iliyo jazwa page zote.
b. Risiti za malipo (bank payin slips)
c. Nakala ya leaving certificate ya shule unakotoka
d. Nakala ya result slip (hati ya matokeo) yako ya kidato cha nne
e. Na mahitaji yote yaliyo orodheshwa Katika ukurasa wa pili na tatu.
f. Nakala ya cheti cha kuzaliwa na passport size moja ya hivi karibuni

Nakutakia kila la kheri Katika maandalizi na tuna mtakia mwanafunzi safari njema kuja BUTUGURI.



NYAMTERELE S CHRISTOPHER

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.

TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

0629896267 (Mkuu wa Shule)
0755196106 (Makamu Mkuu wa Shule)

**FOMU HII IRUDISHWE SHULENI KWA MKUU WA SHULE WAKATI WA USAJILI**

FOMU YA MAELEZO JUU YA MWANAFUNZI

Jina la Mwanafunzi …………………………………………….. liwe jina ulilolitumia Katika shule uliyotoka na utalitumia kwa miaka yote utakayoku wa hapa shuleni na huruhusiwi kulibadili.

Dini…………………………………………Tarehe ya kuzaliwa……………………………………….
Nambari ya kuingizwa shuleni………………Shule aliyotoka.……………………………………………
Tarehe…………………………Michezo uipendayo au shughuli uzipendazo (hobbies) ………………………………………………………………..

Kipimo au historia ya ugonjwa……………………………………………………………

Unaishi na nani/uhusiano…………………………………………………………………

Jina na anwani ya kudumu ya mzazi/mlezi atakayetumiwa ripoti ya maendeleo yakoya kitaaluma na tabia…………………………………………………………………………………………… Kazi ya mzazi/mlezi…………………………………………………………..

Mahali……………………Wilaya…………………………Mkoa…………………………… Habari nyinginezo………………………………………………………………………….. Mzazi/mlezi aliye hai…………………………………………………………………….

Picha nne(4)za wazazi/walezi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

Sehemu hii ijazwe na mzazi/mlezi mwenyewe.

| S/N | JINA | UHUSIANO | NO.SIMU | ANAKOTOKA | KAZI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | | |
| 2 | | | | | |
| 3 | | | | | |
| 4 | | | | | |

Sahihi ya mzazi/mlezi………………………tarehe……………………..simu…………………………

Mimi(jina la mwanafunzi)………………………………..ninaahidi kuzingatia utaratibu, Kanuni na sharia za shule bila kukiuka. Kinyume na hayo hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu. Nitasoma kwa bidi na kufanyakazi ninazotakiwa ili kufikia lengo linalotakiwa.

Sahihi ya mwanafunzi…………………………..tarehe…………………………………..

**FOMU YA MZAZI KUKUBALI MWANAE KUJIUNGA NA KIDATOCHA TANO**

**SHULE YA SEKONDARI BUTUGURI**

1.Mimi…………………….........Baba/Mama/Mlezi wa………………………….. Ninayeishi Wilaya …………………… Mkoa ………………………… nakubali mwanangu…………………… ajiunge na shule ya sekondari ya BUTUGURI Katika mchepuo wa masomo………………………………..aliyochagua yeye mwenyewe.

2. Mimi mzazi/Mlezi wa kijani huyu naahidi kushirikiana na walimu Katika malezi ya mwanangu akiwa shuleni na hata nje ya shule. Kwamba ni wajibu wangu kama mzazi/mlezi kumuhimiza mwanangu asome kwa bidi na afuate sharia na taratibu zote za shule.

3.Kwamba nitalipa ada na michango mingine yote ya shule Katika muda uliopangwa na kwamba kila mwisho wa muhula nitamtaka mwanangu anipe taarifa ya maendeleo yake kitaaluma na tabia. 4.Nakiri nimempatia/sijampatia mwanangu simu aina ya……………….wakati anakujashuleni

.

Jina la mzazi/mlezi………………………………………….

Sahihi…………………………………..Tarehe………………………………………..

BUTUGURI GIRLS' SECONDARY SCHOOL P.O.BOX 1085, MUSOMAMARA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FOR THE STUDENT
(To be filled in the Government hospitals only)

1.Student'sname…………………………………………………..Age………………………

2.Please examine the above mentioned student to her fitness for joining advanced level studies in the following test:-

i. Blood examination Haemoglobin……………………………………………………

ii. Stool examination…………………………………………………….

iv. Bilharziasis………………………………………………

v. Urinalyisis………………………………………………… vi. Tuberculosis Test(TB)…………………………………………….. vii. Eye……………………………………………………. viii. Abdomen……………………………………………………….. viii. Athma…………………………………………………….

viii. Headache…………………………………………………

x. Inability to eat certain type of food……………………………………………………… xi. Skin disease……………………………………………………,

xii. Pregnancy……………………………………………………… xiii. Any abnormalities noted ………………………………………………….. xiv. Any chronic complains noted above…………………………………………………

xvi. Anything else that the school health staff should know about…………………………………

xvii. Any treatment given/recommended………………………………………………………

xviii. Any STD detected……………………………………………………………………

Note: Incase of unhealthy detected, it is recommended that a student should get treatment before coming to school.

I have examined the above student and consider that she is physically fit for joining advanced/ordinary level studies.

Signature of the Examiner…………………………………………………………

Designation……………………………………………………….

Station…………………………………………...

Date…………………………………………………….